

# **International Anglican Family Network**

## **International Anglican Women's Network**

**Jarida la pamoja katika kipindi cha Siku 16 za Uanaharakati dhidi ya Dhuluma za Kijinsia, Novemba 2020**

# **Janga Juu ya Janga**

**Jinsi Waanglikana wanavyochukua hatua dhidi ya kuongezeka kwa unyanyasaji na dhuluma za nyumbani katika kipindi cha COVID-19**



# Janga Juu ya Janga

## Tahariri



*Na Mandy Marshall, Mkurugenzi wa Haki ya Kijinsia katika Afisi ya Muungano wa Waanglikana*

**'Je, yale tunayofanya yanaathirije mahusiano?'** Swali hili ni kichocheo kikuu katika kuchambua jinsi tunavyoendelea katika mchakato wa kuhakikisha kuna ustawi wa binadamu kwa ajili yetu sote. Je, tunachangia katika ukuaji na maendeleo ya familia zetu, marafiki, wenzetu, wakaazi wa parokia na wanajamii kwa matendo na maneno yetu? Au tunafifisha mwangaza ndani kwa yale tunayosema na kutenda? Je, huwa hata tunachangia katika kuwa karibu kuuzima ule mwangaza? Zaburi 139

inatukumbusha kwamba tumeumbwa na Mungu na kwa jinsi ya ajabu. Kila mmoja wetu ni zawadi kwa ulimwengu, tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Katika historia yote ya ulimwengu hakutakuwa na mtu mwingine kama wewe. Sisi ni wa kipee jinsi hiyo. Basi inasikitisha kutambua kiwango cha uchungu na uharibifu unaowapata wanawake wengi na baadhi ya wanaume ulimwenguni kote kutokana na dhuluma za kijinsia (GBV).

Kwa jarida hili, mashirika ya International Anglican Family Network na International Anglican Women's Network yaliamua kuungana pamoja na kutafuta njia za kukabiliana na Dhuluma za Kijinsia (GBV) katika Muungano huo. Mwanamke mmoja mionganini mwa watatu hupitia dhuluma za kimwili/kingono, na kutokana na kuongezeka kwa visa vya dhuluma za nyumbani kila mahali, hili ndilo limekuwa janga juu ya janga wakati wa COVID-19. Simulizi hizo zinatia moyo na zinaonesha hatua mbalimbali zilizochukuliwa, kuanzia hatua ya kidayosisi yenyeye mpangilio mzuri huko Melbourne, hadi kwenye simulizi ya samadi ya minyoo na uwezeshaji wa kiuchumi nchini Bangladesh. Hizi ni hatua tofauti sana za kukabiliana na Dhuluma za Kijinsia na zina matokeo mazuri, zinasisitiza utendaji na zinafaat katika muktadha wake. Ni matumaini yangu kwamba hatua hizo zitakutia moyo kutenda na kuleta mabadiliko kadri unavyoweza na kwa kile ulicho nacho. Tunaweza kujifunza mengi sisi kwa sisi katika Muungano wetu wa Kianglikana.

Kuangazia Dhuluma za Kijinsia kunafanyika katika muda ufaao tunapoelekea katika Siku 16 za Uanaharakati. Kampeni ya kila mwaka inaangazia kazi inayofanywa ulimwenguni kukomesha Dhuluma za Kijinsia na vile vile kazi ambayo bado instahili kutekelezwa. Siku hizo 16 zitaanza mnamo tarehe 25 Novemba hadi siku ya Haki za Binadamu tarehe 10 Disemba. Mwaka huu nimeandaa mfulululizo wa mikutano na mafundisho kwenye mtandao yatakayowashirikisha watu wa ajabu wanaofanya kazi kusitisha Dhuluma za Kijinsia. Jiunge. Habari za kina zinapatikana katika ukurasa wa 18.

Ni fursa kubwa kuandika kama Mkurugenzi wa Haki ya Kijinsia. Nilichukua jukumu hilo mnamo mwezi Aprili mwaka huu wakati wa kipindi cha kukaa nyumbani (lock down) Bado ninasubiri kukutana na wenzangu ana kwa ana au kuketi mezani kwangu afisini. Katika miezi yangu michache ya kufanya kazi nyumbani, niliandika makala yanayohusu, 'Dhuluma za nyumbani na COVID-19: Jinsi Makanisa yanavyoweza kuchukua hatua'. Hii yapatikana katika lugha nyingi kwenye <https://bit.ly/34L7ZJU>. Ipakue, isome na uhakikishe viongozi wako wa kanisa wana nakala.

Tunajua kwamba dhuluma za nyumbani hutokea pia makanisani lakini mara kwa mara zinafunika na kimya, aibu na unyanyapaa. Tunahitaji kuileta nuru ya Kristo katika sehemu hizi zenyenye giza na kuwaonesha upendo, huruma na ukarimu wale waathiriwa wa dhuluma. Alama ya Nne ya Umisionari inatuhimiza kugeuza mifumo isiyokuwa ya haki katika jamii, kipinga kila aina ya dhuluma na kuitafuta amani na upatanisho. Hatuwezi kumsubiri mtu mwingine kuchukua msimamo dhidi ya dhuluma; sote tunawajibu wa kukabiliana na hali hii, tukifanya kazi pamoja kuona kwamba ulimwengu umebadilika.

Maono yangu ni kuona kwamba makanisa yetu yote ni sehemu salama kwa kila mtu. Hatutanyamaza tena au kujifanya hatuoni dhuluma hizo. Hatutatea Dhuluma za Kijinsia kwa kutumia maandiko au kufikiria kwamba ni tatizo lisilotuhusu. Sisi, kama Muungano na kama Wakristo ulimwenguni, tunachukua msimamo na kusema kwamba hili linatuhusu, hili ni kanisa letu. Dhuluma zote za Kijinsia ni makosa na sharti zikome. Je, utajiunga nami katika safari hii, tusafiri pamoja? Wasiliana nami kupitia [mandy\\_marshall@anglicancommunion.org](mailto:mandy_marshall@anglicancommunion.org). Naomba ujue kwamba nitakushangilia!

## **International Anglican Family Network (IAFN)**

Shirika la IAFN linafurahia uwezo kutoka kwa Mungu wa familia kama chanzo cha mahusiano mazuri sana, utambulisho, kukubalika, uanafunzi na upatanisho. Kutokana na kufurahia huku IAFN ni mtetezi wa familia machoni mwa tabia zinazodunisha uwezo huu, na linatoa simulizi za matumaini, na kukuza utunzaji wa familia na kuendeleza familia kama kitovu cha hadhi ya binadamu.

Baruapepe: [iafn@anglicancommunion.org](mailto:iafn@anglicancommunion.org)

<https://iafn.anglicancommunion.org>

<https://www.facebook.com/AnglicanFamilies>

## **International Anglican Women's Network (IAWN)**

Sisi ni sauti ya kijasiri na ya kinabii kwa wanawake wote katika Muungano wa Kianglikana, tunafanya kazi kudumisha hadhi ya wanawake na wasichana waliyopewa na Mungu, na kukomesha ukosefu wa usawa wa kijinsia na dhuluma, na kuendeleza mahusiano ya haki mionganoni mwa watu wote.

Baruapepe: [iawn@anglicancommunion.org](mailto:iawn@anglicancommunion.org)

<https://iawn.anglicancommunion.org>

<https://www.facebook.com/groups/IntAngWomen>

**Picha ya jalada la mbele:** Warsha ya 'Kataa Dhuluma' Lahore, Dayosisi ya Raiwind

## **Yaliyomo**

Wakati Nyumbani si mahali salama.....	3
Kutumia vyombo vyaya habari kuvunja miiko.....	4
Hatua za kishemasi kadri Dhuluma za Kijinsia zinavyoongezeka.....	5
Wanaume kama watetezi na waathiriwa .....	6
'Kanisa la chakula cha jioni' huhamasisha .....	7
Warsha ya 'Kataa Dhuluma.' .....	8
Ubia wa marejesho .....	8
Kupata upya roho ya maisha ('esprit de vie') .....	10
Makaazi ya kukimu mahitaji .....	10
Samadi ya minyoo na hadhi.....	11
Kujenga dayosisi huru kutokana na dhuluma .....	12
Msaada wa kisheria na ushauri nasaha .....	13
Umuhimu wa kushiriki simulizi .....	14
Msaada wa dayosisi wa kujituma .....	16
Siku 16 Tafadhalii jiunge nasi kwenye mtandao.....	17
'Hakuna tena 1 mionganoni mwa 3' .....	18
Kuishi, kumpenda Bwana Yesu, .....	18

## **Wakati Nyumbani si mahali salama**

*Na Hana Kirreh, mwanamke Mkristo mwenye asili ya Kiarabu kutoka Palestina na aliyezaliwa Bethlehemu na kwa sasa anaishi Jerusalemu ambako ni mwanachama wa kundi la washirika wanaoongea Kiarabu katika kanisa kuu la St George.*

Kama vile West Bank na ulimwengu mzima, ugonjwa COVID-19 ulienea katika Yerusalem Mashariki. Kuanzia mwanzoni mwa mwezi Machi, Wizara ya Afya ilipiga marufuku mikusanyiko, mikutano na kufanyia kazi eneo la kazi na watu wakaombwa kusalia nyumbani.

Kutokana na hali hiyo ngumu na watu kukatazwa kwenda hapa na pale, warsha za uhamasishaji na uwezeshaji ambazo kwa kawaida huziendesha na kusimamia kwa ajili ya wanawake Yerusalem Mashariki zimesitishwa kwa sababu za kiafya. Kuzuiliwa kwenda hapa na pale kwa zaidi ya siku 55 mwanzoni mwa janga hili haikuwa rahisi. Kuzuiliwa huku kumerejeshwa tena Yerusalem Mashariki kuanzia wiki ya mwisho ya Septemba, kwa sheria na masharti makali zaidi. Kile kinachofanya hali iwe mbaya zaidi ni kwamba watafutaji wengi wa riziki



wamepoteza kazi zao, hali ambayo imefanya hali ya uchumi iliyokuwa mbaya kuzidi kuwa mbaya, au mapato kupungua.

Kuzuiliwa kwenda hapa na pale kumeleta matatizo ya ziada kwa wanawake wa Yerusalem kama ninavyoamini ndivyo ilivyo kwa wanawake wengi ulimwenguni kote ambao huenda wanapitia hali hizo hizo na wanadhulumiwa. Wanawake wengi wanaishi katika makaazi duni, katika nyumba ndogo na za watu wengi pasipo matuta mazuri wala bustani.

Kukaa nyumbani 24/7 kumesababisha matatizo ya kisaikosojia na kiwewe kwa watoto, jambo linalowaongezea mzigzo wanawake. Kuishi chini ya uvamizi wa Israeli na kulazimishwa kuvumilia athari kadhaa huonekana kuwa uhalisia wa kipekee kwa wanawake wa Kipalestina.

Kuzuiliwa kwenda hapa na pale kuna makali ya aina mbili: hofu ya kuambukizwa virusi na kazi. Katika kisa cha Yerusalem, dhuluma ni suala la kijamii, kiuchumi na kisiasa, hali inayooongeza ukosefu wa haki unaotekelozwa dhidi ya wanawake na wanaume. Lakini bila shaka tunaweza kuona kwamba dhuluma inawalenga wanawake walio hatarini kwa sababu ya jinsia yao.

Kutokana na kikundi changu cha wanawake nimejifunza mengi juu ya mateso yao na shida, ambayo ni pamoja na unyanyasaji wa kingono, wa kimatusi, kihisia na wa kisaikolojia, pamoja na ufinyu wa uchumi unaosababishwa na janga hilo. Mwanamke mmoja alisema, "Kutokana na kutoruhusiwa kwenda hapa na pale, nimepatwa na mfadhaiko, huzuni na kutengwa. Sina hakika hali hii itadumu kwa muda gani na jinsi nitakavyoweza kuyarudia maisha yangu ya kawaida." Alisema warsha na mikutano zimebadilisha maisha yake yakawa mazuri zaidi na sasa kila kitu kimebadilika.

Wengine waliogopa kuongea kwa sababu hapakuweko na faragha nyumbani kwao. Kuongea kuhusu mateso yake kunaweza kutuzwa kwa kutendewa dhuluma. Mwanamke mmoja hakuweza kuongea lakini alifaulu kutuma jumbe za WhatsApp kueleza kuhusu maisha yake ya mateso kila siku chini ya amri ya kutokwenda hapa na pale.

Licha ya taswira hii ya hali ngumu na dhuluma, wanawake wengine walisema kuwa kutoruhusiwa kwenda hapa na pale kunatoa fursa ya kuwa na familia zao, kwa kuwa katika maisha ya kawaida kuwa pamoja sana halikuwa jambo rahisi.

Ili niweze kuwapa msaada wa kimsingi hawa wanawake, niliweza kuwaunganisha wengine na vituo vinavyotoa ushauri nasaha na usaidizi wa kisaikolojia huko Yerusalem Mashariki. Kipindi cha kutoruhusiwa kwenda hapa na pale kitakapokwisha, wanawake hawa na watoto wao wanahitaji kupewa ushauri nasaha wa ana kwa ana ili waweze kushinda madhara ya muda mrefu ya afya zao za kiakili. Kazi nyangi inastahili kufanywa ili kuwasaidia wanawake hawa kunusurika na kuwa na nguvu na ujasiri wa kukabiliana na dhuluma za nyumbani kwa hekima na nguvu.

**Wasiliana na:** Hana Kirreh, [Hzk26669@hotmail.com](mailto:Hzk26669@hotmail.com)

## Kutumia vyombo vya habari kuvunja miiko

*Na Abigail Saidi, Muungano wa Akina Mama (Mothers' Union), Uganda*

Huku Uganda tumekuwa tukipeperusha vipindi vya redio na televisheni kuwahamasisha watu kuhusu Dhuluma za Kijinsia na hususan kuongezeka kwa visa hivyo kutokana na janga la COVID-19. Wakati mpango wa Dhuluma za Kijinsia ulipoanzishwa katika majimbo yote ya Uganda, visa kadhaa ambavyo havikuwa vimeripotiwa vilianza kuibuka. Hii ni kwa sababu kuna itikadi fulani ya kuficha visa vya dhuluma, kwa kuwa ni mwiko kutaja au kumsema mtu yejote ambaye ni mtekelezaji wa dhuluma. Hii ni moja ya itikadi za kitamaduni zinazokabiliwa kuititia kwa mpango huu, kwa lengo la kuona kwamba visa vingi vinarihotiwa na vile vile kuzidisha uhamashajiji wa dhuluma dhidi ya wanawake na watoto katika jamii. Juhudi za makusudi zimefanywa kuititia vipindi vya redio, kujenga hali ya kujiomini katika watu ili waweze kuripoti aina yoyote ya dhuluma kwa mamlaka husika.

Baada ya vipindi kadhaa vya redio, Mratibu wa Maendeleo wa Muungano wa Akina Mama (MU) wa Dayosisi ya Buganda Magharibi alisikia habari za mchungaji mmoja aliyewateka watoto na kuwapeleka nyumbani kwake. Matokeo ya kusikiliza vipindi hivyo, ni kwamba mtu mmoja alihisi amepata nguvu za kujitokeza na kupiga ripoti kuhusu yale aliyosikia kuhusu yule mchungaji. Yule mchungaji alipatikana amewaficha wasichana 25 walio chini ya miaka 18, na kukiuka haki zao kwa kutowapa chakula na vile vile kuwa na uhusiano wa kingono nao. Aliwadanganya wazazi wao kwa kuwaambia alikuwa anawapeleka kusomea shule nzuri baada ya kuondolewa kwa amri ya kutokwenda hapa na pale (lock down). Basi Muungano wa Akina Mama ulipopata habari hizi, tuliweza kushirikiana na maafisa wa polisi ambao walikwenda kumtia mbaroni yule mchungaji na kuwarudisha wale watoto kwa wazazi wao. Kwa sababu tumekita mizizi katika jamii, sasa tunaweza kuzisadia familia kushinda kiwewe hiki kuititia ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia.



Sasa watu wameanza kuona umuhimu wa kupiga ripoti kuhusu visa vya dhuluma. Kuvunjilia mbali itikadi za kitamaduni zinazoendekeza dhuluma kwa wanawake na watoto, kunahitaji juhudu endelevu kuititia vipindi vya redio na mazungumzo ya kijamii ili kukomesha hali hii.

**Wasiliana na:** Naomi Herbert, [Naomi.Herbert@mothersunion.org](mailto:Naomi.Herbert@mothersunion.org)

## Hatua za kishemasi kadri Dhuluma za Kijinsia zinavyoongezeka

*Kasisi Bianca Daews ni mchungaji msaidizi katika Parokia ya Kianglikana ya Good Shepherd huko Salvador Bahia, nchini Brazil. Vile vile yeye ni mwasiisi-mkurugenzi wa Interdisciplinary Group for Gender and Education (GIGE) katika Dom Pedro Segundo University Centre huko Salvador-Bahia. Hapa katika makala yake, anaelezea hatua kadhaa ambazo zimechukuliwa katika kukabiliana na ongezeko la viwango vya Dhuluma za Kijinsia.*

Shirika la Wanawake la Kanisa la Kianglikana la Kiepiskopali Brazil (Episcopal Anglican Church of Brazil) limeandaa hatua kadhaa katika sehemu ya uzuiaji na ukabilianaji wa dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana ambazo zimezidi katika miaka kumi iliyopita.

Mnamo mwaka wa 2011, nyumba ya Casa Noeli dos Santos iliwekwa wakfu huko Ariquemes, Roraima, nyumba ambayo inawapoka wanawake waliodhulimiwa pamoja na watoto wao hadi pale watakoweza kujisimamia wenye kijamii pasipo kuwa katika hatari ya kuuawa. Soma habari zaidi kuhusu Casa Noeli katika ukurasa wa 10.

Tuliandika na kuchapisha vijitabu kuhusu 'Preventing and Combating Gender-based Violence against Women', katika lugha tatu (Kireno, Kiingereza na Kihispaniola), vijitabu hivyo vilichapishwa kwa usaidizi wa *Serviço Anglicana de Diaconia* (SADD). Vijitabu hivi vilizinduliwa katika dayosisi zote na katika wilaya ya umisionari.

Video kuhusu 'Preventing and Combating Gender-based Violence against Women' ziliandaliwa kukimu mahitaji ya wanawake katika mazingira ya dhuluma wakati wa janga la COVID-19. Wanawake waliotawazwa na wale wasiotawazwa kutoka sehemu zote duniani walishiriki katika video hii. Video hizo zilihaririwa katika ubora wa chini ili ziweze kupakiwa katika simu za mkononi za wanawake maskini na walio mbali sana nchini Brazil.

Tulitangaza makongamano manne juu ya 'Jinsia, Dini na Utofauti' na tukawashirikisha viongozi wa dini, viongozi wa harakati za kijamii na wawakilishi wa wasomi. Kongamano hili lilifanyika katika jiji la Salvador-Bahia, na pia tukaandaa kongamano la 'Jinsia, Haki za Binadamu na Ujinsia' huko São Paulo mnamo 2016, ambapo tulizindua jarida lenye kichwa hicho hicho.

Mnambo 2019 tulitafsiri kwa Kireno kitabu cha mwanatheolojia wa Amerika aitwaye Elizabeth Cady Stanton,

kitwacho, 'The Bible for Women (Biblia kwa Wanawake)', na yalikuwa mafaniko makubwa katika masomo ya theolojia ya jinsia na uteteaji wa wanawake.

Kundi la wanawake waliotawazwa na wasiotawazwa walikusanyika pamoja kushiriki neno la Mungu na kuomba pamoja kila baada ya siku 15 kupitia jukwaa la mtandaoni ili waombe kwa ajili ya masuala yanayowaathiri.

Katika kipindi cha janga la COVID-19, tumehusika katika shughuli za muungano wa makanisa, za kisiasa na kibinadamu pamoja na wanawake wa kutoka makundi mengine, kama vile 'Get your Fundamentalisms out of the Way - For the Life of Women' na katika



kukusanya na kupeleka vikapu vyenye bidhaa kwa ajili ya wanawake, hususan akina mama wasioolewa katika pembe za miji ya Salvador na miji mingine ya Brazil.

Tulizindua tovuti ya 'Empower your Sister-Mwezeshe Dada yako', ambayo ni nafasi ya mtandao ambayo lengo lake ni kukaribisha, kujulisha na kuweka wazi shughuli za wanawake wa imani, ndani na nje ya Kanisa la Kianglikana la Kiepiskopali Brazil, kwa lengo la kuwawezesha

kuweza kufikia usawa wa kijinsia, na vile vile kuzuia na kukabiliana na dhuluma za kijinsia, haswa, dhuluma za kidini na za nyumbani zinazotendewa wanawake na wasichana. Website: <https://www.empoderesuirma.com>

## **Wanaume kama watetezi na waathiriwa**

*Kuwakaribisha wanaume katika harakati nchini Zambia*

Matokeo ya janga la COVID-19 yanaanza kudhihirika zaidi na zaidi nchini Zambia. Ripoti za dhuluma za kingono na kijinsia pamoja na ndoa za watoto zimeongezeka. Jamii nyingi nchini Zambia zinakabiliwa na athari za janga huku zikiwa zinazama zaidi katika dimbwi la umaskini. Katika familia hizi zinazokumbwa na matatizo ya kifedha, kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa ajira ya watoto na unyanyasaji wa kingono na dhuluma kwa wanawake na wasichana, isipokuwa hali hii izuiwe.

Wanawake na watoto wamenaswa majumbani mwao pamoja na wale wanaowadhulamu na wametengwa wasiweze kupokea huduma na rasilimali za afya ya ngono na uzazi. Kuzuiliwa kwenda hapa na pale (lockdowns) kumesababisha shule na sehemu nyingine salama kwa wasichana zifungwe, na wasichana kutoweza kuhudhuria vipindi vya ushauri. Wasichana wako katika hatari zaidi ya Dhuluma za Kijinsia, ndoa za watoto, mimba zisizotarajiwa, na maambukizi ya VVU.

Kufanya kazi kufikia kiwango cha usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake na kuwashirikisha wanaume ni jambo la muhimu katika kufikia mafanikio mengi ya maendeleo, pamoja na kupunguza umaskini, kuboresha afya na kushughulikia shida zingine za idadi ya watu. Mahusiano ya wanaume na wavulana kwa wanawake na wasichana yanaweza kusaidia au kuzuia uboreshaji wa afya na matokeo ya maendeleo. Kwa hivyo Baraza la Makanisa nchini Zambia limekuwa likiwashirikisha kikamilifu wanaume na wavulana katika mapambano dhidi ya Dhuluma za Kijinsia.

Baraza liliwafundisha wanaume 10 katika wilaya nne kama watetezi dhidi ya Dhuluma za Kijinsia katika jamii zao. Wanaume hao pia walifundishwa masuala ya kisheria ili waweze kuripoti aina zote za unyanyasaji wa kingono na kijinsia katika jamii zao. Licha ya kuzuiwa kwenda hapa na pale, wanaume wamekuwa wakihamasisha jamii zao kwa kutumia vituo vya radio vya eneo lao.

Wanaume na wavulana wanaweza pia kuwa waathiriwa wa Dhuluma za Kijinsia. Mmoja wa



Mtandao wa wanaume waliofunzwa, Revd Terras, waliweza kumsaidia mwathiriwa wa kiume wa Dhuluma za Kijinsia. Kwa sababu ya COVID-19, Bwana Tembo (jina limebadilishwa) alipoteza kazi na huo ulikuwa mwanzo wa shida nyumbani kwake. Walianza kuwa na changamoto za kiuchumi ambazo zilisababisha mizozo ya kila siku ndani ya nyumba. Siku moja walikuwa na mzozo na mke wa Bw Tembo akamumwagia maji ya moto mumewe.

Rev Terras aliripoti suala hilo kwa kitengo cha Msaada wa Waathirika ambacho kilichukua hatua haraka na mke huyo alikamatwa. Wanandoa hao sasa wamekuwa wakipata ushauri nasaha unaowezeshwa na wanachama wa Mitandao ya Wanaume.

**Wasiliana na:** Kasisi Canon Emmanuel Chikoya, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa nchini Zambia, [chikoya@gmail.com](mailto:chikoya@gmail.com)

## 'Kanisa la chakula cha jioni' huhamasisha

*Kasisi Canon Helen Van Koevering ni Mkuu wa Kanisa la Episkopali la St Raphael huko Kentucky, USA. Kanisa lake linakabiliana na kuongezeka kwa dhuluma za nyumbani wakati wa janga hilo.*

Mnamo Oktoba 2019, gavana wa jimbo la Kentucky alizungumzia juu ya 'viwango vya janga' la dhuluma za nyumbanii katika jimbo hilo, na vurugu za watu wawili walio na uhusiano wa karibu kama sababu ya asilimia 46 ya visa vya kuwadhulumu na kuwatelekeza watoto. Sasa, katika miezi kadhaa iliyopita ya COVID-19, makazi ya waathirika wa dhuluma za nyumbani yanaripoti kuongezeka kwa dhuluma kama matokeo ya kutengwa, ukosefu wa ajira na usongo. Nambari za simu za moja kwa moja zinaripoti ongezeko la asilimia 9 za mawasiliano ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha 2019, na asilimia 10 ya wapigaji simu wakitaja athari za COVID-19 kama hali waliyopitia.

Uhitaji wa ufahamu wa umma na msaada kwa waathirika ni muhimu sana.

Wakati kamati ya umisionari ya Kanisa la Episkopali la St Raphael ilipopanga mpango wetu wa 2020, hatukuwa tumezingatia ni nini kitatokea mnamo 2020. Kwa miaka miwili, tulikuwa tumefanya "Makanisa ya Chakula cha jioni" kila mwezi kwa wastani wa watu 45 kukusanyika kwa sherehe ya Ekaristi kwenye meza zilizoja sadaka za vyakula, na kushiriki mazungumzo juu ya masuala yanayohusiana na haki - mazungumzo ambayo hayawezekani kila wakati muda wa kunywa kahawa katikati ya ibada za Jumapili.

Tulikuwa tumeamua kuwa na kaulimbiu ya 'Uponyaji kwa Familia zilizo katika Mazingira Hatarishi' katika mfululizo wa milo mitano ya Kanisa la Chakula cha jioni, na kuyaangazia mashirika matano ambayo yalito msaada kwa wanawake na watoto wapone kutoptana na mazoea mabaya, ulangizi wa watu kwa ajili ya ngono, umaskini, kufungwa, na kutafuta usaidizi wa kisheria. Wote walichukulia Dhuluma za Kijinsia kama jambo lililowahu wote. Kusudi letu lilikuwa kuinua sauti za waathirika waliopona, kuongeza ufahamu mionganoni mwa wale waliohudhuria Kanisa la Chakula cha Jioni, na kuzingatia mwitiko wetu wa kanisa na wa Kikristo.



Kisha vikwazo vya COVID-19 vikabisha hodi. Na mipango yetu iligeukia kuwa ukuzaji wa mfululizo wa mahojiano ya mada fulani ya Kanisa la Chakula cha Jioni na kutafakari masuala ya kitheolojia pamoja na mashirika hayo yote. Na, kama samaki na mikate iliyobarikiwa na Yesu, idadi iliyohusika iliongezekwa hadi wastani wa 150 kila jioni.

Teknolojia pamoja na mioyo iliyo na ari ya haki, ya umisionari na wanawake na watoto walio katika mazingira hatari, imewezesha tuweze kuwafikia wengi zaidi, kuwamasisha watu na kuwasaidia. Pia ilisababisha mashirika kuandaa video ambazo sasa huzitumia wanapotafuta kuendelea kuwashudumia kutoka mbali waathirika wa dhuluma.

**Wasiliana na:** Helen Van Koevering, [revhelen@sreclex.org](mailto:revhelen@sreclex.org)

Kipindi cha Chakula cha Jioni kilichorekodiwa kinapatikana kwenye <https://youtu.be/RmsIJzZFaWQ>

## Warsha ya 'Kataa Dhuluma.'

Amal Sarah anaishi Lahore, nchini Pakistan na anafanya kazi kama mtu wa kujitolea katika Women Development & Service Society (WDSS), Dayosisi ya Raiwind, Kanisa la Pakistan. Anasoma katika Chuo cha Forman Christian College (Chuo Kikuu Kilichoidhinishwa), anasomea shahada yake ya M.Phil katika Sayansi ya Mazingira. Anaandika na kusema hivi:

Kama sehemu ya huduma ya WDSS, inayofanya kazi ili kuinua jamii, kujenga uwezo, uhamasishaji wa afya na kusisitiza maswala ya kijamii, warsha ya siku moja juu ya Uhamasishaji wa Dhuluma za nyumbani ilipangwa ifanyike 30 Septemba 2020. Kauli mbiu ya warsha hiyo ilikuwa 'Kataa Dhuluma' - hatua ya kuzuia dhuluma na ukatili wa nyumbani. Watu themanini na tisa kutoka katika jamii ya eneo hilo, wakiwemo wanafunzi, washirika kutoka parokia tatu za dayosisi, na wanagenzi katika ukunga na wanagenzi wa magonjwa ya akili katika jamii kutoka Kituo cha Kurekebisha tabia cha WDSS walishiriki.



Wakati wa amri ya kutotoka kwenda hapa na pale ya COVID-19, kulishuhudiwa kuongezeka kwa dhuluma za nyumbani, na visa vya ubakaji wa wanawake na watoto viliongezeka nchini Pakistan. Kwa hivyo tulikusanya jamii ya eneo hilo katika jukwaa moja ili kuwashamasisha miongoni mwao. Vikao juu ya dhuluma za nyumbani, ukatili dhidi ya wanawake, na wanaume na unyanyasaji wa watoto/visa vya ubakaji, viliendeshwa na wafanyakazi wa WDSS na timu ya watu wa kujitolea. Sababu ambazo zimesababisha dhuluma hizi kuongezeka na kuzorotesha mshikamano wa jamii zilisisitizwa. Washiriki walipangwa katika makundi ili kufanya shughuli fulani na waliombwa

kupendekeza suluhisho jinsi tunavyoweza, kama watu binafsi, kanisa na jamii, kuchukua jukumu muhimu katika kuzuia aina mbalimbali za dhuluma zinazotokea katika jamii ya Pakistani. Katika moja ya shughuli za kikundi, vifungu mbalimbali vya Biblia vilishirikishwa washiriki juu ya dhuluma za nyumbani na wakapewa nafasi ya kuvitafakari na kuhusisha marejeo ya Biblia kwa hali iliyopo sasa katika jamii. Warsha nzima ilikuwa ya majadiliano na imekuwa nafasi salama, ambapo sio tu shida ziliangaziwa, bali pia ililenga kutafuta suluhisho ili angalau kuchukua hatua ndogo katika kuanda mazingira ya amani na utangamano.

**Wasiliana na:** Amal Sarah, [amalsarah78@yahoo.com](mailto:amalsarah78@yahoo.com);  
<https://www.facebook.com/wdssdioceseofraiwind1989/>

## Ubia wa marejesho

Kutoka kwa Ven Dr Lyndon Drake, Shemasi Mkuu wa Tamaki Makaurau (Auckland) na mwenyekiti wa Te Whare Ruruhau o Meri, Wakala wa Huduma ya Jamii wa Kanisa la Kianglikana la Maori katika Mkoa wa Kiepiskopali wa Aukland.

Aotearoa / New Zealand ni maarufu kwa uzuri wake wa asili. Jambo lisilojulikana sana ni kwamba pia ni nchi yenye viwango vyake vya juu vya umaskini wa watoto na madhara ya kifamilia, ikiwemo Dhuluma za Kijinsia.

Katika huduma yangu huko Auckland / Tāmaki Makaurau, sikusoma tu juu ya takwimu za eneo hilo. Ninaona athari kwa maisha ya watu katika huduma yangu ya kila siku.

Kanisa la Anglicana katika nchi yetu limefanya juhudii kubwa kutambua tofauti katika utendaji wa huduma kati ya Wamāori (watu wa asili wa Aotearoa / New Zealand) na makundi ya makabila/na tamaduni nyingine. Muktadha wangu wa huduma haswa ni mwa Wamāori. Wamāori wanaathiriwa zaidi na madhara ya kifamilia kuliko makundi mengine ya watu katika jamii. Watu wengi ninaowajua na kuwajali katika parokia zangu wameumizwa na madhara ya familia, au ni watekelezaji wa madhara ya familia.

Ndani ya mazingira yetu ya Anglicani ya Wamāori, kituo chetu cha kazi ya jamii kinaitwa Te Whare Ruruhau o Meri ('Nyumba ya Makao ya Mariamu'). Kama jina linavyopendekeza, kilianzishwa na utambuzi maalum wa

madhara yanayosababishwa na dhuluma za kijinsia. Katika miaka ya hivi karibuni, Whare mara nyingi kimechukua neno pana, 'madhara ya familia', kutambua kwamba dhuluma za kijinsia ndio hali inayojitokeza zaidi katika tabia kama hizo mbaya katika makundi ya familia.

Katika mwaka uliopita, kituo cha Whare kilifanya kazi kwa karibu na zaidi ya 3,000 *whānau* (familia) kutokana na watu kuwatuma kwetu. Familia kwa ujumla hutumwa kwenye kituo cha Whare na kitengo cha kusimamia haki ya jinai. Visa vya kudhuru familia vimeongezeka katika miezi ya hivi karibuni, na vimechangiwa na athari za kiuchumi za COVID-19 na hali ya kutoruhusiwa kwenda hapa na pale inayohusiana na janga hilo. Familia nyingi za Wamāori ziko katika hatari ya matatizo ya kutoka nje, kwa sababu ya athari za ukoloni na mfumo wa ubaguzi wa rangi.

Moja ya vipengele muhimu vya kazi ya Whare ni kwamba tunawenza kuepuka kutumia mfumo wa baba, kwa sababu kama Wamāori tunadhibiti muundo na yale maudhui ya msaada ambao familia zilizo katika mazingira hatarishi zinahitaji.

Kama matokeo, kazi yetu na ufadhili imekua kwa kasi katika miaka miwili iliyopita, maana mtindo tunaotumia kwa Wamāori umeleta matokeo bora tunapoingilia kati katika mazingira magumu sana. Kazi ya Whare imesababisha idadi kubwa ya watoto na watu wazima walio katika mazingira hatarishi kulindwa kutokana na madhara zaidi.

Changamoto ya kufanya kazi kwa kiwango kikubwa kwa msingi wa rufaa ni kwamba Whare mara kwa mara kilikuwa na mawasiliano yake ya kwanza na nyumba moja muda mrefu baada ya hatari ya madhara kudhihirika. Kwa mfano, visa vingi vya kijinsia hufichuliwa nje na wito wa polisi. Inaweza kuchukua muda kwa sehemu zingine za serikali, kama Idara ya Sheria, kujua ripoti ya tukio la polisi na kuamua kwamba rufaa ya kwenda Whare ilikuwa inafaa.

Katika miezi michache iliyopita, tumekuwa sehemu ya ushirikiano mzuri sana na mashirika kadhaa tofauti, na haswa na polisi. Jeshi la polisi la eneo hilo lilifanya makubaliano na kituo cha Whare na mashirika mengine kukodisha jengo moja pamoja kwa muda. Ghorofa ya juu inatumiwa na wafanyakazi wanaoshughulika na madhara ya familia katika eneo la kusini mwa Auckland. Ghorofa ya chini inatumiwa na Te Whare Ruruau o Meri na mashirika mengine. Jengo hilo limepewa jina na Askofu wetu na kuitwa *Te Taanga Manawa*, jina ambalo linamaanisha moyo wa watu ambao mashirika yanawasaidia, na moyo wa Mungu unaowaelekea binadamu.



Wakati kisa cha madhara ya familia kinapowafikia polisi, wafanyakazi wa kijamii wa kituo cha Whare wanawenza kutumwa mara moja, na kuna uwezekano mkubwa waathiriwa kupokea msaada wa mapema. Polisi wamekuwa vyombo vya ukombozi, si utoaji wa adhabu tu.

Tunawenza kuendelea kuwa na sauti ya kipekee ya Kikristo katika harakati zetu za kijamii. Hii kwa kiasi fulani ni kwa sababu hali ya kiroho inatambuliwa kama sehemu muhimu ya maisha katika kielelezo cha afya na maisha ya kawaida ya kijamii nchini Aotearoa / New Zealand. *Te Whare Tapa Whā* ('nyumba iliyo na kuta nne'), ni jina linalotokana na jinsi Wamāori wanavyochukulia ustawi wa kibinafsi na wa kijamii, kuwa na hali ya kiroho kama moja ya 'kuta' zake nne. Bila kuingilia imani za kibinafsi, kuna kiwango fulani kinachokubalika kwa ajili ya kujihusisha na mambo ya kiroho.

Wakati huo huo, umahiri wa Wamāori unaoletwa na Te Whare Ruruau o Meri ni mzuri sana kiutekelezaji, na hutofautisha kazi yetu na ile ya mashirika kadhaa yasiyokuwa ya kidini.

Vipengele hivi viwili vya thamani na vya muda mrefu vya mchango wa Te Whare Ruruau kwa jamii vimepata maoni mapya katika ushirikiano wetu wa mashirika mengi huko *Te Taanga Manawa*. Ninaamini tumbahatika kupata njia isiyo ya kawaida ya kuleta matunzo kwa wale walioathiriwa na madhara ya familia au

wanaotekeleza madhara ya familia, na ushirikiano na polisi, asasi za serikali, na mashirika mengine yasiyo ya serikali, kuonyesha nia ya Kikristo ya kuuponya uliopondeka.

**Wasiliana na:** Ven Dr Lyndon Drake, [lyndon@tetaitokerau.anglican.org](mailto:lyndon@tetaitokerau.anglican.org)

## Kupata upya roho ya maisha ('esprit de vie')

*Marthe Vira, ambaye anaishi Kinshasa, ndiye Mratibu wa Maendeleo ya Jamii ya Muungano wa Akina Mama katika Jimbo la Kanisa la Anglikana la Congo. Anaelezea jinsi akina dada watatu wamesaidiwa kufuatia dhuluma waliyotendewa.*

Adele, Celeste na Estelle (majina yamebadilishwa) ni ndugu. Kabla ya janga la COVID-19 kuja, waliweza kulipa kodi katika eneo lao. Walikuwa wakienda masokoni kama wachuuzi wa samaki na viungo. Siku moja, mume wa Celeste aliwaomba shemeji zake wamkopeshe dola 100 na akasema atawalipa na riba ya dola 20. Wakakubali kufanya hivyo.

Sasa, wakati wa kipindi cha kuzuiliwa kwenda hapa na pale (lockdown), yule bwana hakuweza kulipa ile hela aliyokopa. Wale akina dada walipomwendea yule bwana na kutaka kulipwa pesa zao, aliwapeleka mahali pa faragha ambapo kulikuwa na watu wachache na, pamoja na kikundi cha wavulana na wanaume wakubwa wahalifu (wanaoitwa hapa Kinshasa 'KULUNA'), walianza kuwashambulia. Waliwaacha bila nguo na wakiwa wamejeruhiwa.

Mwanamume huyo pia alienda nyumbani kwa wale akina dada, na kuwapora wanawake hawa watatu mali zao zote. Wale wanawake walikuwa katika shida, wakilia kila siku, bila matumaini ya maisha au 'esprit de vie-roho ya maisha'. Lakini tulipoanza mradi wetu unaohusu Dhuluma za Kijansia, mwanaharakati mmoja wa jinsia aliyefundishwa katika kutafuta waathirika aliwapeleka afisini kwetu. Aliwashauri, akawaombea na kuwapa vifaa vya kuwasaidia. Akina dada hao sasa wanapona esprit de vie yao na wameanza tena kurudia shughuli zao za kila siku.

Wanawake hao wanamshukuru Mungu kwa kazi zote ambazo Muungano wa Akina Mama wa jimbo la Kinshasa unafanya kupitia idara ya jimbo ya Muungamo wa Akina Mama kwa kushirikiana na Mary Sumner House nchini Uingereza, kuwasaidia manusura wa Dhuluma za Kijinsia katika kipindi hiki kigumu cha COVID-19.

**Wasiliana na:** Marthe Vira, [marthevira1@gmail.com](mailto:marthevira1@gmail.com)

## Makaazi ya kukimu mahitaji

*Miongoni mwa Alama tano za Azimio la Muungano wa Kianglikana ni 'Kushughulikia mahitaji ya binadamu kwa kupenda huduma' na 'Kubadilisha miundo isiyo ya haki ya jamii, kupinda dhuluma za kila aina na kufuata amani na upatanisho' Hizi zinachangia utaratibu ulioandalialiwa katika manispaa ya Ariquemes - RO katika Kanisa la Kiepskopali la Anglikana la Brazil (IEAB) wilaya ya umisionari (inayojumuisha majimbo ya Rondônia, Mato Grosso na Mato Grosso do Sul), kupitia kazi ya kishemasi ya makao ya Noeli dos Santos kwa wanawake walio katika hali za dhuluma za nyumbani.*

Makaazi ya Casa Noeli yalianzishwa kama jibu kwa hitaji la mahali hapo, ambapo wanawake ambao walikuwa wakipitia dhuluma za nyumbani hawakuwa na mahali salama pa kwenda. Mahali pazuri palihitajika kukidhi hitaji hili na kwa hivyo parokia ya Santíssima Trindade, iliyowakilishwa na kasisi wao, Revd Elineide Ferreira

Oliveira, ilikabiliana changamoto hiyo. Walihamasisha watu wa eneo hilo na kuunda taasisi ya kisheria ili stakabadhi zote muhimu kwa shirika la uhisani ziweze kufanywa kuwa rasmi.

Kazi sasa imekuwa ikitekelezwa kwa miaka tisa kupambana na dhuluma dhidi ya wanawake, na leo mradi huo umetambuliwa kieneo, kiserikali, kitaifa na kimataifa kama kitabu cha marejeo katika kupambana na aina zote za dhuluma dhidi ya wanawake.

Wanawake wanapewa mahali salama, na kutofichua sehemu wanayokaa, na wanapata huduma kupitia mashirika ya umma ambayo ni mahali pa kuingilia katika utunzaji wa



wanawake walio katika mazingira ya dhuluma. Katika makaazi ya Casa Noeli, huduma za utunzaji hutolewa, asilimia 100 bila malipo, kwa kipindi cha siku moja hadi 90, pamoja na huduma ya kisaikolojia. Rufaa hufanywa kwa taasisi zenye uzoefu, kama vile afya, elimu, mahakama, soko la ajira na kozi za kitaaluma, kuhakikisha kwamba wanawake wanaokaribishwa na Casa Noeli wanaondoka wakiwa wamewezeshwa iwezekanavyo na hivyo kuwa na nguvu za kushinda dhuluma walizopitia.

Makaazi ya Casa Noeli, ambayo ndiyo taasisi ya pekee katika Bonde lote la Jamari linalojumuisha manispaa ya Ariquemes na manispaa nyingine tisa, yamehudumia jimbo hili lote, yakikuza sera mpya za umma na kuboresha zile ambazo tayari zipo.

Nyumba hiyo inatunzwa na taasisi ya kisheria ya *Associação Anglicana Desmond Tutu*, ambayo inapokea misaada kutoka kwa washirika wa ndani na wa kimataifa kupitia *Serviço Anglicana de Diaconia* (SADD). Rasilimali nyingine zinatokana na fedha za manispaa kupitia ushirikiano na utawala wa umma. Ushirikiano huu ni muhimu sana kuwezesha Casa Noeli kuendelea kufanya kazi kikamilifu, ikizingatiwa kwamba kuna gharama nyangi zinazohitajika.

Wanawake wanakaribishwa na watoto wao na wanapewa bidhaa za usafi wa kibinasi, chakula na dawa, pamoja na nguo zilizotolewa, kwa sababu wengi hufika tu na nguo walizovaa, na pia wanapewa misaada mingine.

IEAB imejitokeza katika mapambano dhidi ya dhuluma dhidi ya wanawake, ikiwa ni mfano kwa makanisa mengine ambayo pia yameamshwa na hitaji la kukabili na kushughulikia suala hili ambalo limekuwa likijidhihirisha katika jamii kwa uzito mkubwa. Unyanyasaji wa nyumbani ni shida ya kiafya ya umma inayoathiri viwango vyote vya matabaka ya kijamii, rangi, imani na makabila.

Viongozi wa dini wamejaribu kuingiza katika huduma zao vitendo vinavyoendeleza mjadala na kushughulikia mada hii ya dharura ambayo ni lazima kukabiliwa na jamii nzima. Na ni kwa njia hii ya kuthibitisha imani yetu ndipo, kama kanisa, tunaendelea kujiweka kama sauti ya kinabii na kuifanyia kazi injili ya Mungu inayohubiriwa katika majengo ya makanisa yetu. Tunawapa sauti wale ambao wamenyamazishwa na tunawahakikishia hadhi na haki wale ambao wamefanywa wasionekane na ni wanyonge. Tunafanya hivi kwa hakika kwamba pamoja tunaweza kubadilisha hali hii ambayo inatuathiri sisi sote kama Wakristo.

**Wasiliana na:** Revda Elineide Ferreira Oliveira, [elineideieab@hotmail.com](mailto:elineideieab@hotmail.com)

## Samadi ya minyoo na hadhi

*Hadithi hii kutoka kwa Kanisa la Bangladesh inaelezea jinsi uwezeshejaji wa kiuchumi wa mke ulisaidia kupunguza shinikizo kwa wanandoa na kusababisha uhusiano wenye amani zaidi.*

Kalabati na mumewe Stephan wanaishi wilaya ya Rajshahi, Bangladesh. Hawana shamba lao wenywewe. Stephan analima shamba kwa kukodisha kwa muda mfupi kutoka kwa mwenye nyumba na familia yake inaishi kwa shida sana. Wana watoto wawili wa kiume wanaosoma shule ya msingi.

Familia hiyo haikuwa na amani. Umaskini uliongezeka kwa sababu ya shida ya kuzuiliwa kwenda hapa na pale kutokana na janga la COVID-19 na walikuwa wakigombana. Kalabati alikabiliwa na ukatili wa kikili na wa kimwili. Ingawa alifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya familia yake, hakuweza kupata pesa za kuchangia mapato ya familia.

Mnamo Oktoba 2016, Kalabati alijiunga na Kikundi cha Maendeleo cha Gandharaja cha Shalom, kitengo cha maendeleo cha Kanisa la Bangladesh. Kama mwanachama, anapewa mafunzo juu ya masuala mbalimbali, pamoja na mafunzo ya samadi ya minyoo. Sasa yeche huandaa mbolea ya vermi (kwa kutumia minyoo katika taka zilizooza) kwa msaada wa kifedha kutoka Shalom.

Wakati wa kuzuiliwa kwenda hapa na pale kutokana na COVID-19 mwaka huu, Kalabati amelima patal (maboga yenye ncha) kwa kutumia mbolea ya vermi katika desimali tisa za ardhi, na kutoa mavuno mengi sana. Kufikia sasa, ameuza Takas elfu 12 za patal kutoka kwenye bustani yake ya jikoni. Zao hilo linaweza kuuzwa kwa mwezi mmoja zaidi na kuna uhitaji mkubwa katika soko la ndani. Bei ni nzuri kwa sababu mboga hiyo ni tamu na yenye virutubishi. Watu huuliza, mbona kuna mavuno mengi namna hiyo? Kisha Kalabati huwajibu na kusema, "Ni uchawi wa samadi ya minyoo!" Htuambia huku akitabasamu, 'Tunaweza kuokoa mapato kadhaa kutoka shambani na kuyatumia kwa ajili ya familia. Ninaweza kutumia pesa hiyo kuwasomesha watoto wetu

vizuri. Vile vile Ninaweza kukimu mahitaji yangu mwenyewe. Watu wawili katika familia wanapoleta mapato, huwa kuna amani."

Uzalishaji wa mapato umeongeza heshima na hadhi ya wanawake, kwa hivyo tunaishukuru sana Shalom. Dhuluma za nyumbani zimepungua kuitia shughuli ndogo za kiuchumi. Majirani wanajifunza kutoka kwa familia hii jinsi ya kuishi kwa amani na kupunguza umaskini, wakizingatia mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira kwa kupunguza mbolea za kemikali na dawa za wadudu.



**Wasiliana na:** Prodip Chand Mondal, Katibu wa Mratibu, Afisi ya Sinodi katika Kanisa la Bangladesh, [pcmondalcob@gmail.com](mailto:pcmondalcob@gmail.com)

## Kujenga dayosisi huru kutokana na dhuluma

*Na Daniela Gennrich, Kanisa la Kianglikana la Afrika Kusini*

Huduma ya Jinsia ilianza katika Dayosisi ya Natal mnamo 2017 wakati nilipoteuliwa kama Lay Canon kwa ajili ya Jinsia na Dhuluma za Kijinsia na Askofu mwenye maono Dino Gabriel. Wakati huo alikiri kwangu kwamba "sijui chochote, lakini najua kwamba huu ni wito wa Mungu kwa Dayosisi. Ninakutegemea wewe unifundishe".

Tulianza kwa kutuma kidadisi kwa wadau wote, lakini kidadisi hicho hakikuleta matokeo mengi. Askofu aliandaa mikutano minne ya Wachungaji kuhusu Jinsia na Dhuluma za Kijinsia mnamo 2017 hadi 2019. Wengi walijawa na ari- lakini mazungumzo yalikuwa yameanza.

Vijana katika wilaya moja walitoa changamoto kwa uongozi wa dayosisi kuelezea ni kwa nini ulimwengu haukuwa mahali salama chini ya uangalizi wetu. Waliongoza Jumapili ya kuvalia Mavazi Meusi mnamo 2018.

Mwanzoni mwa 2018, nilisema wazi wasiwasи wangu kwamba tulikuwa tukiongea kuhusu Dhuluma za Kijinsia kana kwamba zinatendeka 'huko nje' bila kuzingatia uadilifu wetu wenyewe wa ndani. Askofu Dino alikuwa mtu wa kufanya maamuzi sana. Aliitisha mkutano na waandishi wa habari, ambapo alitangaza kwamba Dayosisi hiyo ilikuwa na sera ya kutovumilia kabisa aina yoyote ya utovu wa nidhamu ya kingono au nyingine. Aliwaalika manusura watoe ripoti kwake. Wengine walifanya hivyo, na tukachunguza visa hivyo tukitumia 'Vigezo vya Kichungaji' vya Kanisa la Anglikana la Kusini mwa Afrika. Michakato mingine ilikamilishwa na haki ilitendeka; wengine walifadhaika na kubaki hawajakamilika wakati wa kipindi cha mapumziko katika dayosisi yetu.

Wakati huo huo, mashemasi wengine wakuu walisaidia kupeleka mazungumzo kwenye ngazi ya parokia, na nilikutana na timu zingine tarajiwa za parokia.

Baada ya kujuzulu mapema kwa Askofu Dino, kazi ya kijinsia ilisimama kwa muda. Msaidizi wa askofu Forbes Maupa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Askofu kunisiaidia kushikilia huduma ya jinsia.

Kisha ikaja COVID-19 na amri ya kuzuiliwa kwenda hapa na pale (lockdown). Makasisi kadhaa walisimulia juu ya shida zao za kusaidia familia kwa mbali.

Mapema Juni, mwanachama wa Muungano wa Akina Mama (MU) na ambaye alikuwa mke wa mchungaji alidaiwa kujiuwa kwa kukata tamaa baada ya miaka mingi ya kuteswa katika ndoa. Kwa msaada kutoka kwa uongozi wa Muungano wa Akina Mama wa dayosisi, niliitisha mkutano wa wake wa wachungaji, wanawake wengine na pamoja na wana timu wa Huduma ya Jinsia. Tuliwasikiliza wakisimulia yale waliyopitia, tukazungumza juu ya njia za kutatulia shida hizo, na tukatoa mapendekezo maalum ya hatua zinazofaa kuchukuliwa, ambazo baadaye ziliidhinishwa na Tawi. Lakini kisha, mume aliuawa. Tukaanza tena upya kutafuta suluhisho. Viongozi wa Ushirika wa Akina Mama wa Anglikana walishirikiana kushughulikia mahitaji mengi ya watoto.

Niliombwa nisimamishe kazi tena. Mnamo Julai tulituma mwaliko kwa watu wa kujitolea kuwa sehemu ya kujenga dayosisi ya siku zijazo isiyokuwa na dhuluma. Sasa tuna timu ya makasisi zaidi ya 30, wana ndoa, washiriki wa Tawi, vijana na waumini wa parokia.

Timu tofauti zinaongoza shughuli halisi zifuatazo:

- Uandikajii wa Kauli ya Dayosisi juu ya usawa wa kijinsia, haki na Dhuluma za Kijinsia, ambayo inatambulisha anwani ya barua pepe ya kutolea malalamiko: [safechurch@anglicansa.org.za](mailto:safechurch@anglicansa.org.za). Kauli hii imejikita katika Mkataba wa Usalama wa Jimbo na Kanisa Jumuishi.
- Utengenezaji wa video inayoonesha kuwa Dhuluma za Kijinsia haziko 'huko nje' lakini ziko karibu kabisa, na kampeni ya mitando ya kijamii inayotegemea video hiyo kuanzisha mazungumzo na kuwaelekeza watu kwa Huduma ya Jinsia na kwa Kanisa Salama na Jumuishi.
- Timu ya Huduma ya Wanaume inatoa Mafundisho ya Biblia yanayozingatia Muktadha ya kila wiki kuitia WhatsApp kwa wanaume wanaoshughulikia maswala ya usawa wa kijinsia na Dhuluma za Kijinsia, na waliandaa kikao cha kwanza cha Wanaume kuitia Zoom.
- Kikundi cha Mafundisho ya Bibilia ya Wanawake yanayozingatia Muktadha kinawezesha masomo mawili kwa makasisi wa kike na wanafunzi wa uchungaji, na kinapanga mfululizo wa mafundisho ya Biblia kwa ajili ya wanawake wengine, ili kuwasaidia kudai sehemu za Biblia ambazo zinathibitisha hadhi yao, wito na uongozi, kwa msingi wa theolojia ya Kiafrika ya kuwatetea wanawake.
- Jinsia si tu juu ya *yaliyomo* lakini pia *mchakato*: Mfululizo wa fursa za siri za ushauri nasaha wa mtandaoni kwa vikundi vidogo vya wachungaji ambao hawajaoa au kuolewa na wana ndoa unakusudia kuwasaidia katika kukabiliana na matatizo yanayotokana na COVID-19 na matatizo mengine makubwa katika Dayosisi.
- Mimi ni mwanachama hai wa timu ya Makanisa ya Jimbo yaliyo Salama na Makanisa Jumuishi. Tunaendelea kuhamasisha watu kuripoti visa vya unyanyasaji wa kingono na tumeanza kutafuta mikakati kadhaa ya kukinga.
- Uongozi wa Shirika la Wanawake wa Dayosisi wanapanga warsha kuhusu Dhuluma za Kijinsia na Kanisa Salama kwa ajili ya washirika wao.
- Tunachunguza matumizi ya teknolojia ili kuanzisha huduma ya habari ya mtandaoni na ikiwezekana nambari ya kuitisha msaada.

Kinachosisimua zaidi ni kwamba timu mpya ya Huduma mpya ya Jinsia ina mambo mengi, na kwamba shughuli zaidi na zaidi zinajitokeza kutoka ngazi ya chini kadri parokia chache zinafunguka na kuanza kuzungumzia Dhuluma za Kijinsia. Kwa mfano, mafundisho ya mtandaoni kuhusu Dhuluma za Kijinsia yanaongozwa na Ushirika wa Wanawake wa Anglikana katika parokia moja, wengine wameandaa ibada zinazoangazia Dhuluma za Kijinsia, na wengine wana Maazimio ya Ujumuishaji.

Tunazo hadithi nydingi za kusimulia na masomo mengi ya kuwaambia. Hili ni eneo gumu na lenye changamoto! Kasisi Mkuu na Tawi wanaunga mkono kikamilifu. Lakini wakati mwengine kumekuwa na upinzani na hali ya kurudisha nyuma. Wakati mwengine hatusikizani vizuri kama wana timu, na lazima tuanze kusikizana tena, Hatuko karibu na mahali ambapo tunaamini Mungu anataka tuwe. Lakini tumekubali kusafiri pamoja, na mapungufu yetu yote na udhaifu, na katikati ya matatizo mengine mengi chini ya COVID-19.

Nimejifunza kuwa huduma inayowezesha inahitajika, huduma ambayo inakubali kwamba sisi sote tumo safarini, inahibitisha jukumu la kila mtu, na inafungua fursa kwa ajili ya maoni yote yenye uwezekano wa kufanyiwa majoribio, lakini pia ni huduma ambayo inatuita sisi wote kuwajibika ndani ya mfumo wazi wa maadili na kanuni zinazotokana na Maandiko na uzoefu.

**Wasiliana na:** Daniela Gennrich, [coordinator@wwsosa.org.za](mailto:coordinator@wwsosa.org.za). Daniela pia ni mratibu wa muungano wa We Will Speak Out Afrika Kusini <http://www.wwsosa.org.za>

## Msaada wa kisheria na ushauri nasaha

*Chama cha Undugu cha Delhi (DBS) kilianzishwa mnamo 1973 na Undugu wa Nyumba ya Watawa ya Ascended Christ huko Delhi, India. Kinjalenga kuhudumia maskini na wale waliokandamizwa, bila kujali tabaka, imani au kabilia, na kinafanya kazii haswa mionganii mwa wazee, wanawake na vijana kutoka katika jamii zinazoteseka ili kuendeleza maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi kuitia elimu, makao, mafunzo ya stadi, utetezi wa sheria na ubia.*

*Katika mifano miwili ifuatayo ya hatua na msaada wa kisheria uliochukuliwa na DBS, majina ya watu wote yamebadilishwa.*

Hemani mwanafunzi wa chuo alikutana na Aruj katika hafla fulani. Wakawa marafiki na kuanza kukutana mara kwa mara. Aruj alikuwa akimwomba Hemani wakutane sehemu tofauti tofauti. Baada ya mikutano kadhaa, alianza kuwa karibu naye kimwili. Alipokataa, alisema kwamba alitaka kumuo na kwamba ukaribu huu wa mwili ulikuwa kawaida kabla ya ndoa. Hii iliendelea kwa karibu mwaka mmoja na mwishowe, Hemani alipogundua kuwa hatamuoa, aliacha kukutana naye. Pia alikuja kujua baadaye kuwa Aruj alikuwa ameo na alikuwa na mtoto mdogo. Alikuwa amewafanya vivyo hivyo wasichana wengine. Aruj alisisitiza kwamba Hemani anapaswa kukutana naye kwa mara ya mwisho ili wasuluhishe mizozo yote iliyokuwa kati yao. Basi wakakutana na akambaka. Ndipo Hemani akapiga simu kutumia namba ya usaidizi wa DBS na baada ya muda akakutana na mtu wa kujitolea wa DBS.



Wanachama wa Mahila Panchayat (baraza lisilo rasmi la mji wa wanawake linalohusika na uingiliaji kati wa shida na msaada wa kisheria katika ngazi ya jamii) inayoendeshwa na DBS, walihusika na, huku wakisaidiwa na polisi na mawakili, waliwasilisha malalamiko. Hemani alitibiwa na Ripoti ya Kwanza ya Habari ikawasilishwa. Sasa kesi iko kortini na inaendelea kusikizwa.

Wanachama wa Panchayat hufanya ufuutiliaji wa mara kwa mara na kumsaidia Hemani kwa shughuli zote za stakabadhi na mahitaji mengine.

Mume wa Janya hakumfanya mazuri, kwa hivyo, baada ya miaka tisa ya ndoa, alirudi kwao kwa

kuzaliwa kuishi na mama yake na watoto wake wawili wadogo. Wakati alipokuwa akiishi na mama yake, mumewe alikuwa akimtembelea na, baada ya siku chache, wangezozana na kumpiga Janya kabla hajaondoka. Janya aliendelea kuishi na mama yake na binti zake wawili.

Siku moja Janya alimwacha binti yake wa miaka saba Urmi peke yake ndani ya nyumba wakati akifanya kazi ya ujakazi katika nyumba za karibu. Mama yake alikuwa amempeleka binti yake mkubwa kumwona daktari. Janya aliporudi nyumbani, alimwona Urmi analia kwa maumivu makali kwenye sehemu ya chini ya tumbo lake. Pia alikuwa akiuja damu. Janya alimkimbiza mtoto hospitali ya karibu ambapo alitibiwa na daktari. Aliporudi nyumbani, Janya alimuuliza Urmi amueleze kile kilichotokea. Akasema kuwa kijana wa jirani alikuwa amemchukua kwenda kununua chokoleti kisha akampeleka mahali mbali na kumnajisi. Alipopiga yowe, alimwambia anyamaze vinginevyo atamwua na kumwacha hapo. Urmi alimuahidi kwamba hatamwambia mtu ye yeyote na akamrudisha nyumbani.

Hali ya Urmi ilizidi kuwa mbaya na kutokwa na damu hakukuwa kunaisha licha ya kupokea matibabu. Janya alimpigia simu jamaa yake ambaye alikuwa akiishi Delhi, ambaye alimfahamu mshauri nasaha kutoka DBS. Alimwagiza Janya ampeleke mtoto huyo mara moja mijini Delhi. Alipokuwa huko, Urmi alipelekwa katika Hospitali ya Guru Teg Bahadur, ambayo inashirikiana na Namba ya Dharura ya DBS ya Kuwasaidia Wanawake. Alitibiwa huko kwa ajili ya madhara ya ndani na maambukizi aliyopata. Kesi hiyo iliwasilishwa na sasa iko kortini.

Wakati huo huo, Urmi mepata afueni sasa na anaishi na mama yake. Anaendelea kupokea ushauri nasaha na atapelekwa shule wakati zitakapofunguliwa.

**Wasiliana na:** Fr Solomon George, [delhibrotherhood@gmail.com](mailto:delhibrotherhood@gmail.com) Delhi Brotherhood Society:  
<https://www.delhibrotherhood.org>

## Umuhimu wa kushiriki simulizi

*Kasisi Moumita Biswas wa Kanisa la Kaskazini mwa India anaandika juu ya mipango miwili huko Asia inayoshughulikia masuala ya Dhuluma za Kijinsia wakati wa janga la COVID-19: warsha ya mtandaoni na tamasha.*

Mnamo Septemba mwaka huu, viongozi 36 wanawake wa kanisa walishiriki kwenye warsha ya mtandaoni yenye kichwa 'Wanawake Wanaochangia Amani Pamoja' Wanawake walismulia hadithi zao za changamoto,

matumaini na uvumilivu, na wakajadiliana jinsi wanavyofanya kazi kumaliza Dhuluma za Kijinsia wakati wa hili janga.

Warsha hiyo iliandaliwa na 'Chakula Huongea Hadithi yake ya Upendo na Mtando wa Matumaini'. Mtando huu umeunda jukwaa ambalo viongozi wa kanisa wanawake wa Asia wanaweza kushiriki mikakati, kujenga uhamasishaji, kudhihirisha mshikamano, kufarijana wakati wa uchungu, kulea hali ya kiroho ya upendo na haki, na kuimarishe mitando ili kumaliza Dhuluma za Kijinsia na kushughulikia maswala ya uhakika wa chakula na haki ya hali ya hewa.

Wakati wa semina ya mtandaoni tulijifunza mengi sana kutoka kwa kila mmoja wetu. Kwa mfano, viongozi wa Ushirika wa Wanawake nchini Bangladesh wanasaidia wafanyakazi wa kiwanda cha nguo (sana sana wanawake) katika kipindi cha njaa na kutoa chakula na vifaa vya msaada ikiwa ni pamoja na barakoa na vifaa vya kijikinga kibinafsi.

Viongozi wanawake wa kanisa huko Pakistan wanashughulikia maswala ya dhuluma za nyumbani na kuwezeshana kuvunja ukimya, na masomo ya Biblia mtandaoni na kwa kusaidiana wakati wa kiwewe na uchungu.

Viongozi wanawake wa kanisa huko Nepal wanafanya kazi katika jamii kuziwezesha familia kukomesha ndoa za lazima za utotoni ambazo zimeongezeka wakati wa janga hili. Mtoto wa Kike anachukuliwa kama mzigo huko Asia Kusini.

Nchini Sri Lanka, ambapo wanawake ndio msingi wa uchumi, Bodi ya Wajibu wa Kijamii ya Dayosisi ya Anglikana ya Colombo imepatia kipaumbele afueni ya wanawake na watoto ambao ndio walio hatarini zaidi wakati huu wa janga. Wanaangazia pia kujenga familia zenye nguvu, za kujitegemea, na endelevu na kusaidia juhudzi za ujasiriamali za wanawake


Wakati wa janga hilo, vimbunga vya mara kwa mara nchini India na Bangladesh vinavyotokana na mabadiliko ya hali ya hewa vimeharibu maisha ya watu na makaazi ya kiasili. Wanawake hao walismulia hadithi kuhusu mipango ya kanisa ya kujenga jamii na makanisa endelevu, kupanda miti, kurejesha maisha na kuwawezesha watu wa vijiji kukuza 'bustani za virutubisho' au bustani za jikoni, na kupanda mboga za kusaidia familia.

Wakati wa semina hiyo ya mtandaoni, viongozi wa kanisa wanawake pia walijadili mikakati ya kukuza Siku 16 za Uanaharakati na, baada ya kusikia juu ya Tamasha ya Amani ya Haki ya Jinsia inayoahdimishwa sasa na baadhi ya waumini huko Lahore katika Dayosisi ya Raiwind, Kanisa la Pakistan, watalenga kuanzisha sherehe kama hiyo katika makanisa na nchi zingine.

Alyssa Saleem ndiye mwanzilishi wa Tamasha la Amani ya Haki ya Jinsia huko Lahore, inayoanza tarehe 1 Oktoba hadi 10 Desemba. Kulingana na habari za tamasha, "Oktoba ni muhimu sana kwetu kujihusisha katika kampeni na mipango mbalimbali ya kukomesha Dhuluma za Kijinsia na kukuza haki ya kijinsia. Mnamo Oktoba tunazingatia Uhamasishaji wa Dhuluma za Kinyumbani na mwezi wa Saratani ya Matiti, ulimwengu unaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa ya Mtoto wa Kike, na Siku 16 za Uanaharakati ni Novemba. Kwa hivyo tunaanzisha aina mbali mbali za utetezi ili kukuza haki ya kijinsia."

Kama ilivyo katika sehemu nyingi za ulimwengu, Dhuluma za Kijinsia zimeongezeka nchini Pakistan wakati wa janga hili la COVID-19. Uvamizi wa nzige miezi michache iliyopita umesababisha umasikini, njaa, kufa njaa na dhuluma za nyumbani. Wanawake, wasichana na watoto ndio walio hatarini zaidi.

Kanisa la St Peter huko Lahore liliandaa warsha ya uhamasishaji kwa vijana mwezi Oktoba yenye kaulimbiu ya 'Paka Rangi ya Zambarau kwa Kusudi', kwa kuwa rangi ya zambarau inatumwiwa katika kampeni ya kumaliza dhuluma za nyumbani. Vijana hamsini, wa kiume na wa kike, walishiriki. Mbinu iliyotumiwa ilikuwa kuchora bango, ikifuaatiwa na majadiliano, kutafakari kulingana na muktadha na kuliweka Biblia katika muktadha.



Kusimulia hadithi ni mbinu muhimu ya kuvunja ukimya. Ushirika wa Wanawake wa Kanisa la Kumbukumbu la St Esther walifanya sherehe ya kuleta chakula kwa wanawake mwezi Oktoba. Wanawake viongozi wa makanisa wenyenye umri wa miaka 24 hadi 60 walihudhuria. Wanawake walialikwa kusimulia hadithi kuhusu jinsi wanavyokabiliana na janga la korona na dhuluma wanazokabiliana nazo majumbani mwao. Walikula chakula pamoja na kupendana na kutafakari juu ya kisa cha kubakwa kwa Tamari na kaka yake wa kambo Amnoni, ambaye alitumia vibaya nguvu na mamlaka yake (2 Samweli 13). Viongozi wanawake waliileta hadithi hiyo katika muktadha wao. Walijadili mikakati ya kukuza uhamasishaji kati ya wanafamilia na kulinda wasichana, wanawake na watoto katika familia zao na jamii.

**Wasiliana na:** Revd Moumita Biswas, [moumita.iawn@gmail.com](mailto:moumita.iawn@gmail.com)  
 Food Speaks Herstory of Upendo and Matumaini MTANDAO,  
<https://www.facebook.com/groups/642836063000842>

## Msaada wa dayosisi wa kujituma

*Na Robyn Andréo-Boosey, Meneja wa Programu, Kuzuia Dhuluma dhidi ya Wanawake, Dayosisi ya Melbourne*

Kiini kile kinachotuunganisha katika imani yetu ya Kikristo ni onyesho kuu la Yesu la upendo kwa vitendo Katika maisha yake yote, Yesu aliguswa kutenda na upendo wake kwa watu ambaa walikuwa wanateseka na kutengwa, akiwarejeshea utimilifu na kupinga udhalimu uliowanyang'anya heshima yao waliyopewa na Mungu. Katika 2018, kama ishara ya kujitolea kwake kwa kina kushughulikia shida ya dhuluma dhidi ya wanawake, Dayosisi ya Melbourne, Australia, ilianzisha Programu ya Kuzuia Dhulumai Dhidi ya Wanawake na kuteua Meneja wa Programu.

Kufanya kazi kushirikiana na mashirika ya maslahi ya Anglicana, Anglicare Victoria, Brotherhood of St Laurence na Ralationship Matters, Mpango huo unakusudia kusaidia na kuwaandaa viongozi wa makanisa na jamii ziweze kushughulikia na kuzuia dhuluma dhidi ya wanawake.



dhuluma dhidi ya wanawake ndani ya makanisa yao. Kwa hiyo mradi huu unalenga kuiandaa Dayosisi na viongozi wa makanisa kushughulikia swala hili kwa:

- kutoa mafunzo juu ya kutambua dalili za dhuluma, kushughulikia ufhuzi wa dhuluma, na kuwatuma watu kwenye huduma za msaada wa kitaalam. Tunajitahidi kujumuisha hili katika mafundisho ya msingi yanayotolewa na vyuo vya kitheolojia kwa ajili ya viongozi wa baadaye katika Kanisa
- kuunda sera ya dayosisi, taratibu na miongozo kuhusu jinsi ya kukabiliana na dhuluma za kifamilia na kuwasaidia watu wanaozipitia
- kuanzisha jukumu la Mtetezi wa Usalama wa Familia katika parokia ili zifanye kazi pamoja na makasisi. Mtetezi ni kiongozi na muumini aliyefundishwa ambaye huwa mtu wa kuwatemeblea watu na kuzungumza juu ya dhuluma za familia. Anajua jinsi ya kusaidia watu ipasavyo na kuwapeleka kwenye huduma za kitaalam
- kusaidia makanisa kutambua na kuungana na huduma zao za dhuluma za kifamilia ili wajue wapi wanaweza kupata ushauri wa kitaalam na wapi kwa kuwatuma ili wasaidiwe
- kutengeneza rasilimali za kanisa kama mabango ya kupambana na dhuluma yenye nambari za simu za

Maono yetu ni kuona Australia ambayo wanawake na wasichana wanaweza kuishi wakiwa huru kutokana na dhuluma na hofu ya dhuluma-maono ya ujasiri yaliyokita kwenye uhamamu kwamba Mungu anafanya kazi mionganoni mwetu kuleta uponyaji, urejesho na haki katika maisha yetu na katika jamii zetu zote.

Viongozi waliowekwa wakfu na waumini wa kawaida wanahitaji kuandaliwa vyema ili waweze kuwashughulikia watu wanaokumbana na dhuluma. Viongozi wa kanisa mara kwa mara ni mionganoni mwa watu wa kwanza wanaofahamishwa juu ya hali za

kuitisha usaidizi.

Kusaidia watu wanaopitia dhuluma ni muhimu sana. Hata hivyo, hatua yetu haipaswi kuishia hapo. Tunahitaji kuchukua hatua za kuzuia maonevu ya dhuluma kabla hayajaanza. Kuzuia dhuluma dhidi ya wanawake kunahusu mabadiliko ya utamaduni, na kuangalia kupita hali ya visa vya kibinafsi ili kuelewa viwezeshejai vipana vya kijamii ambavyo vinachochera na kuchangia kwa kiasi kikubwa dhuluma dhidi ya wanawake. Kama Wakristo, na sote kama Kanisa, tunalazimishwa na upendo wa Kristo kuondoa utamaduni huu. Viongozi wa kanisa wanawenza kunyoosha imani za watu, mitazamo na tabia zao, na kuwa na fursa za kuleta athari nzuri katika jamii pana, kama vile kwa vikundi vya kucheza michezo, shughuli za vijana na maandalizi ya ndoa. Kwa hivyo tunatafuta kuandaa dayosisi na viongozi wa makanisa wasaidie kuzuia dhuluma dhidi ya wanawake kwa kutoa:

- mafunzo juu ya viwezeshejai vya kijamii ambavyo vinachochera na kuchochera viwango vikubwa vya dhuluma dhidi ya wanawake, na jinsi ya kukabiliana navyo
- ushauri/mafundisho kwa viongozi wa kanisa ili kuwapa nafasi ya kutafakari yale wanayojifunza na jinsi ya kuyatumia katika parokia zao
- nafasi za msaada wa watu wa rika moja kwa ajili ya viongozi waweze kushiriki mawazo na rasilimali zao
- rasilimali za kufundishia mpango wa Mungu wa usawa katika parokia, pamoja na usawa katika vikundi vya mafundisho ya Biblia, vile vile pamoja na huduma ya vijana na watoto
- vifaa vya kujitathmini vya kanisa vya kusaidia parokia kutafakari juu ya utendaji kazi wao na utamaduni wao na kutambua sehemu zozote ambazo huenda pasipo kukusudia wanatoa ujumbe usiosaidia au wenye madhara juu ya thamani sawa ya wanaume na wanawake.

Kumpenda jirani yetu kunamaanisha kukubali kwamba dhuluma na ukatili si mambo MAZURI na tufanye kila tuwezalo kukabiliana na dhuluma hii na kuweka mfano tofauti wa kumwiga Kristo.

**Wasiliana na:** Robyn Andréo-Boosey, [pvaw@melbourneanglican.org.au](mailto:pvaw@melbourneanglican.org.au)

## Siku 16 Tafadhali jiunge nasi kwenye mtando

Umealikwa kwa furaha kushiriki katika hafla nne za jopo la kimataifa na semina tatu za mtandaoni za majadiliano wakati wa Siku 16 za Uanaharakati, iliyoandaliwa na Mandy Marshall, Mkurugenzi wa Haki ya Jinsia katika Afisi ya Muungano wa Kianglikana.

Kwa habari za kina na viunganishi, tazama <https://bit.ly/34L7ZJU> na ufuatilie kwenye mitando ya kijamii:  
@AnglicansEndGBV @AnglicanWorld @AnglicanUN  
<https://www.facebook.com/groups/IntAngWomen>  
<https://www.facebook.com/AnglicanFamilies>

**Saa zote zilizotolewa ni za GMT/UTC**


### Mikutano ya jopo

1. Kushughulikia Dhuluma za Kijinsia katika Muungano wa Kianglikana -Jumatano tarehe 25 Novemba 11.30 asubuhi
2. Kushirikisha Wanaume kumaliza Dhuluma za Kijinsia-Ijumaa tarehe 27 Novemba 2.00 alasiri
3. Theolojia na Maombi: Jinsi theolojia yetu inavyotushirikisha na kutuhamasisha kutenda-Jumatano tarehe 2 Desemba 12.30 mchana
4. Utetezi na Haki ya Jinsia-Alhamisi tarehe 10 Desemba (Siku ya Haki za Binadamu) 2.00 alasiri

### Mafundisho ya mtandaoni kuhusu dhuluma za nyumbani

*Chagua saa zinazokufaa:*

1. Alhamisi 26 Novemba 06.30 asubuhi
2. Ijumaa tarehe 27 Novemba 10.30 asubuhi
3. Jumatatu tarehe 30 Novemba 7.00 usiku



Pakua hii rasilimali ya Kianglikana hapa <https://bit.ly/34L7ZU> or email [mandy\\_marshall@anglicancommunion.org](mailto:mandy_marshall@anglicancommunion.org)

## 'Hakuna tena 1 mionganoni mwa 3'

Muungano wa Akina Mama umetengeneza kifurushi kipyä cha rasilimali kwa zile Siku 16 za Uanaharakati 2020, na vifaa vingine kwa Siku yao ya kwanza ya Siku ya Ulimwengu ya Utendaji Duniani mnamo tarehe 5 Desemba. Pakua kwenye <https://bit.ly/2IU38h9>. Muungano wa Akina Mama -Ireland umetengeneza Shajara ya Maombi ya Siku 16 kwa matumizi haswa wakati wa janga la COVID-19, ambalo limefunua 'janga juu ya janga' la dhuluma za nyumbani. Nchini Ireland, Shirika la Women's Aid limeshuhudia ongezeko la asilimia 43 ya simu zinazopigwa kwenye nambari zao za kuitisha usaidizi tangu Machi 2020. Pakua shajara ya Maombi hapa [www.mothersunion.ie](http://www.mothersunion.ie).

## Kuishi, kumpenda Bwana Yesu,

Tunakukumbuka kama mtetezi na Mwokozi wa wanawake ambao walipitia dhuluma na aibu, Yule aliyenena kwa niaba yao kurejesha hadhi na usalama. Tunakumbuka unasikiliza watoto ambao watu wengine walitaka kuwanyamazisha na kuwafukuza.

Na sasa tunawaleta kwako wale katika jamii zetu ambao wanaishi kwa kuogopa watu wa karibu ambao hutumia dhuluma kwa njia zote kudhibiti na kuwatawala.

Tunaomba msamaha kwa zile njia ambazo Kanisa wakati mwengine limewezesha dhuluma na kuwanyamazisha watu wengi sana, kwani wakati tumeangalia kando, na kumuunga mkono mhalifu, tuliwarudisha watu kwenye sehemu ambazo si salama kabisa.

Bwana Yesu, tupe masikio ya kusikia. Tusaidie kuzingatia, kuunda tamaduni za usalama, kusema ukweli, na kuwa na neema ya kuwa macho.

Tunaomba haya kwa ajili ya kanisa letu, na kwa Kanisa kila mahali. Amina.

*Kirsten Campbell, Dayosisi ya Melbourne, Australia*

Maoni ya wachangiaji binafsi hayawakilishi maoni ya IAFN au IAWN.